# MIGUUNI PA YESU

***Kumtafuta Roho kwa ajili ya kuishi maisha Matakatifu.***

Siku 30

*"……..Naye alikuwa na umbu lake aitwaye mariamu, aliyeketi miguuni pake Yesu akisikiliza maneno yake"* (Luka 10:39)

# *MIGUUNI PA YESU*

*Kumtafuta Roho kwa ajili ya kuishi Maisha Matakatifu.*

Mwongozo wa kuwepo mbele za Bwana kila siku.
Na Saju

Hutolewa na:  Huduma ya Jesus Mission, India.

Toleo la kwanza
Novemba 2009
Imechapishwa na
Graphic Systems & Co. Mallappally

Toleo la kiswahili  Septemba 2011
nakala za Kiswahili- Tanzania
na Assemblies of God Press -Dar es salaam

Jarada na: Joshy John

SAJU JOHN MATHEW
Valilyavattappara, Kuriannor P. O.,
Thiruvalla, Kerala   689 550 INDIA

Phone:+91 469 2672310
Cell:  +91 944 7172310
Email: jesusmission@gmail.com

Imetafsiriwa katika Kiswahili na:
Gospel Campaign Centre, Tanzania, East Africa
Na Rev. Moses Magembe (Senior Pastor)  Na Mr. Peter Busene.

*Copyright © Jesus Mission India*
*Hairuhusiwi kunakili kitabu hiki bila ruhusa ya mwandishi na siyo kwa biashara*



Bwana akajibu akamwambia, "Martha, unasumbuka na kufadhaika kwa ajili ya vitu vingi; Lakini kinatakiwa kitu kimoja tu, na Mariamu amechagua fungu lililo jema, ambalo hataondolewa." (Luka 10:41-42)

Katika ulimwengu wenye mila na desturi zinazobadilika na kuanguka, wakati ambapo watu wanagombania anasa za papo hapo, tunatamani kumwona mtu ambaye atasimama Imara, kusema na kuishi kwa ajili ya mambo ya Milele

Yesu alisema, Mambo mawili yatadumu Milele. Moja ni hazina yako unayojiwekea Mbinguni (Mathayo 6:19-20) na lingine ni muda unaoutumia miguuni pa Yesu (Luka 10:42)

Unapotumia utajiri wako, fedha yako, afya, ushawishi na zaidi ya yote muda wako kwa ajili ya wengine, unajiwekea hazina Mbinguni. (Marko 10:21) Je nini kinatokea unapotumia muda wako ukiwa miguuni pa Yesu? Unashusha Umilele hapa duniani.

Muda wako pamoja na Bwana ni sawa na umilele. Unapokaa miguuni pa Yesu ni sawa na Milele hapa duniani. Ndiyo maana muda tunaoutumia miguuni pa Yesu ni wa thamani kuzidi na kupita hata ile thamani ya ujira wa utumishi wetu kwa ajili ya Bwana.

Katika kizazi ambapo watu wanashauku na masumbufu kuhusu vitu vingi, ni wakati muafaka tukaketi miguuni pa Yesu. Tunapokaa miguuni pake, si tu tunasema naye lakini anasema na sisi pia. Anatukaribisha ndani katika makao yake (Yohana 15:4) Neno lake litatupeleka hadi kwenye ulimwengu wake. Atatujulisha mambo makubwa na yaliyositirika ambayo hatukuyajua (Yeremia 33:3). Tutakaa katika uwepo wake na burudiko lote (Zaburi 84:1-2)

Haya ni mafundisho maalum ya kuweko mbele za Bwana. Ninatumaini yatakuwa msaada kwa ajili ya kujitoa kwako katika maombi na kutafakari. Siyo tu kwa ajili ya kusoma tu bali ni kwa ajili ya kutafakari na kuwa na ushirika wa kukaa miguuni pa Yesu. Ebu na tufurahie milele hapa na kujizoeza kwa ajili ya wakati ujao, tutakapoishi pamoja na Bwana Arusi wetu Milele na Milele

SHALOM,
Saju.

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Keti Chini na Uhesabu Gharama Kwanza.**

**Kifungu cha kusoma:** Luka 14:25-35.

*"Maana ni nani katika ninyi, kama akitaka kujenga mnara, asiyeketi kwanza na kuhesabu gharama, kwamba anavyo vya kuumalizia"* ***Luka 14:28-29***

Ramu alizaliwa maskini. Alikuwa na kazi ndogo kwenye duka la bidhaa ndogo ndogo (bidhaa za vyakula na matumizi ya nyumbani). Maishani mwake, alikuwa na ndoto ya kujenga nyumba yake mwenyewe. Alinunua kiwanja kwa kutumia akiba yake yote.Na kwa kutumia fedha za kukopa alijenga msingi wa nyumba ya vyumba vitatu vya kulala. Kwa hali hiyo, kazi ya kujenga msingi ilipokwisha, hakuwa na fedha za kuendeleza hiyo nyumba. Akajikuta katika dimbwi la umaskini kwa sababu kwa wakati huo huo alipoteza kazi yake ya ajira. Mke wake na watoto walikuwa hawana chakula. Kwa kushindwa kulipa kodi ya nyumba kwa miezi mingi, ilibidi aondoke na kutoka kwenye nyumba aliyokuwa akiishi. Mwisho wa yote akahamia kwenye hema iliyokuwa karibu na "msingi" wake wa nyumba aliokuwa ameuweka kutokana na ndoto yake ya kuwa na nyumba; na hilo pia alisaidiwa na baadhi ya watu wema. Watu waliokuwa wakipita pale walilitazama lile hema na kunong'onezana wakisema; "Inasikitisha sana, mtu huyu hakuketi na kuhesabu gharama kabla ya kuweka msingi!"

Kufanyika mwanafunzi wa Yesu ni sawa na kujenga nyumba. Unahitaji kupoteza matofali, saruji, mbao, na jasho ili kujenga nyumba. Vivyo hivyo, imekupasa kupoteza faraja, mali, na nafasi au cheo ili kufanya nyumbani pa milele kuwa halisi.

Yesu akasema, "kama utanifuata, keti na uhesabu gharama utakayopaswa kulipa. Baba yako, mama yako, mke na watoto, ndugu wa kiume na wa kike wanaweza kukuacha kwa sababu ya kuniamini mimi. Ninataka kuona kwamba unaniweka mimi mbele/kwaza, na sio wazazi, mwenzi wako, au ndugu! **(Mstari 25&26).** Vivyo hivyo, yeyote kati yenu asiyeacha vyote alivyonavyo hawezi kuwa mwanafunzi wangu (**mstari 33**)."
Unapaswa kulipa gharama hizi zote kama unatka kuwa mwanafunzi wa Yesu. Hakuna kitu kinachoweza kujengwa bila kupoteza kitu fulani. Hata hivyo, iko thamani kubwa. Kwani kinachopotea sio kitu ukiinganisha na tunachotarajia kupata.

**Maombi:** *Bwana, ninaamua kuuchukua msalaba wangu, kujikana nafsi yangu na kukufuata wewe. Wewe ni Bwana wangu, na ni kila kitu kwangu. Nisaidie kuelewa kwamba vitu ninavyovipoteza hapa ni hazina yangu ya milele…..Amen.*

**Kwa usomaji zaidi: Mathayo** 10:32-39; Luka 19:1-10.

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Wingu Kubwa la Mashahidi.**

**Kifungu cha Kusoma: Waebrania 11:1-12:1**

*Basi na sisi pia, kwa kuwa tumezungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila aina ya mzigo, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu.* ***Waebrania 12:1***

Fikiria umepewa kukimbia mbio ndefu na njia ikiwa imesogwa sana katikati. Ukiangalia lengo ambalo linaonekana kutofikiwa, kabisa unaogopa kutokufanikiwa. Mara anatokea mtu ambaye anakutia moyo. Anakukumbusha kuwa wewe sio mwazilishi. Wengi wamekwisha maliza mbio kwa uaminifu. Anakusihi utazame sehemu ambayo waliotangulia wamekaa wakikutazama ukikimbia. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania ni aina ya mtu huyo anayetia moyo.

Katika sura zilizotangulia, alikuwa akielezea maisha ya hao watakatifu. Anaanza na Abel, hadi kwa Nuhu, Ibrahim, Musa na hamalizi orodha kwa sababu ni wengi. Nami niseme nini tena ? Maana wakati usingenitosha kuleta habari za Gideoni, na Baraka, na Samsoni, na Yeftha, na Daudi, na Samweli na za manabii.
***Waebrania 11:32.***

Kustahimili mateso, dharau, na aibu, wote walisimama kwa ajili ya Mungu. Walikimbia mbio vyema na wakavipiga vita vizuri. Habari zao zimeandikwa katika biblia ili kututia moyo. Mwadishi haongelei habari zao tu, bali pia anatuambia kuwa wanayatazama mashindano yetu kwa shauku kubwa ya kuuona ushindi wetu. Wapo sehemu ya juu kwenye viti kama watazamaji kuwa tunapochoka, wanainuka na kututia moyo kwa ushuhuda wa maisha yao. Tunapodhania kuwa tuko peke yetu na hakuna aliye upande wa Mungu, Eliya atasimama na kutuambia kuhusu habari ya kufundishwa kwake na Mungu kuhusu mabaki ya Mungu. Tunapodhania matatizo ni kama milima mbele yetu, Yoshua atainuka na kuelezea kuanguka kwa ngome za Yeriko. Nehemia atasema juu ya ujenzi wa ukuta ambapo Daniel ataeleza juu ya usiku ule aliokuwa kwenye tundu la simba.

***Maombi:*** *Bwana ninakushukuru kwa ajili ya wingu kubwa la mashahidi, wa nyakati za biblia na hata wa siku za leo, wanaonitia moyo katikamashindano haya. Ninafahamu lengo bado sijalifikia. Japokuwa safari ni ngumu, nisaidie kumaliza mwendo wangu kwa uaminifu. Amen!*

**Kwa usomaji zaidi: warumi 4:18-25; 2 wakorintho 5:6-10.**

**Jione Mwenyewe Katika Mtazamo Wa Mungu**

**Kifungu cha kusoma: Isaya 6:1-8**

*Ndipo niliposema, Ole wangu! Kwa maana nimepotea;kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona mfalme,BWANA wa majeshi.* ***Isaya 6:5***

Katika maono ya Isaya, maserafi hawakuweza kusimama au hata kutazama utakatifu wa Bwana wa majeshi. Kama viumbe wenye nguvu kama maserafi hawakuweza kusimama mbele za utakatifu wa Bwana, mimi je nawezaje, mtu mwenye midomo michafu? Isaya aliona shaka hakujidhania ya kuwa yu hai. Alikuwa ni nabii wa Bwana, na siku zote alitoa ole kwa wengine. Machoni pake alikuwa akijiona mtu bora kuliko watu wengine waliomzunguka. Lakini, alikuwa akijitazama kwa kujilinganisha na wengine. Na sasa kwa mara ya kwanza anajiangali katika mwanga wa Ki-Mungu na hakuridhika. Tutajijua sisi ni nani pale tu tutakapojiangalia katika mtazamo wa Ki-Mungu. Petro alipojiona katika nuru ya Bwana, alilia: Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi Bwana! **Luka 5:8**

Ingawa isaya alikuwa nabii wa Bwana, alikuwa tayari kukubali dhambi zake. Aliungama dhambi zake, na kusema ole wangu! Kwa maana nimepotea! Kwa maana mimi ni mtu mwenye midomo michafu, alilia (**Isaya 6:5**). Kukiri kwake kulipindua mambo yote chini, juu, mmoja wa maserafi wale aliruka juu ya madhabahu akiwa na makoleo mawili yenye kaa la moto. Akagusa midomo yake na kusema, uovu wako umeondolewa kwa sababu kaa hili limegusa midomo yako. Dhambi zako zote zimesamehewa. (Isaya 6:5)

Kama Isaya asingekuwa tayari kukiri dhambi zake, asingesamehewa kamwe. na asingekuwa na uwezo wa kutokutenda  dhambi. Wengi wetu tunajiridhisha. Tunashindwa kumwona Mungu, au kujitazama katika mtazamo wa Ki-Mungu. Hatuoni hatia yetu. Hatuwi tayari kukiri dhambi zetu. Kwa hiyo tunaishi maisha yasiyo na msamaha.

***Maombi:*** *Bwana, hebu nijitazame katika mtazamo wako.. Ninatubu dhambi zangu. Niguse midomo yangu, macho yangu, mikono na nafsi yangu na moto wa madhabahuni. Hatia yangu yote iteketezwe na moto wako-Amina.*

***Kwa usomaji zaidi: Walawi 20:26; Luka 5:6-11***

Siku ya 4

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Kuwa mfu kwa Mambo ya Ulimwengu: Kuwa Hai Kwa Ufalme wa Mungu**

**Kifungu Cha Kusoma: Luka 9:57-62**

*Yesu akawaambia, waache wafu wawazike wafu wao; bali wewe enenda ukautangaze ufalme wa Mungu.* ***Luka 9:60***

Yesu alipowaita wanafunzi wake, mara moja waliacha kila kitu na kumfuata yeye. Lakini hapa, tunamwona mtu mmoja anayeomba muda zaidi. Alisema angemfuata Yesu, lakini ni baada ya kumzika baba yake. Udhuru wake unaonekana ni wa kweli sana. Hata hivyo Yesu hakuwa tayari kusubiri. Ni huzuni iliyoje? Unaweza kusema Ni kwa nini Bwana wetu ni mgumu kiasi hiki, hata asimruhusu huyu kwenda kumzika Baba yake?

Tatizo ni hili. Baba yake alikuwa hajafa bado. Kulingana na mila za kiyahudi, watoto walipata urithi wao pale tu baba yao anapokuwa amekufa. Huyu kijana alitaka kumfuata Yesu lakini hakuona usalama wa kufuatana na kundi la wafuasi wa Yesu. Wote walikuwa ni masikini. Aliwaza ni vema angejiunga baada ya kupokea urithi wake. Na hii ingemhakikishia usalama wa maisha yake. Kwa hili basi ingelimpasa kusubiri hadi pale baba yake atakapofariki.

Yesu akasema, waacheni wafu wawazike wafu wao,; bali wewe enenda ukautangaze ufalme wa Mungu. Waliokufa wa kimwili, kwa kawaida, hawawezi kuwazika wafu. Hapa, Yesu anatumia lugha ile ile aliyoitumia yule kijana. Kwake yeye mazishi ya baba yake yalimaanisha fedha au urithi na fedha ilimaanisha usalama wake. Kwa upande wake, Yesu alikuwa akimaanisha: Ee ndugu, umeitwa kuhubiri injili kwa sababu unaishi kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Watu wale, kaka zako na jamaa zako, ni wafu katika ufalme wa Mungu, waache basi wafu (katika ufalme wa Mungu) wachukue urithi wa baba yako atakapofariki. Wao wanaishi kwa ajili ya wingi wa mali. Ninataka wewe uwe mfu katika wingi wa mali, bali uwe hai katika ufalme wa Mungu. Nenda ukauhubiri ufalme wa Mungu.

Wengi wanaotaka kumfuata Yesu leo, wanasubiri baba zao wafariki. Yesu hakubaliani na wale wanaomtaka Mungu na mali nyingi pamoja. Kama unataka kumfuata unatakiwa kwanza uyafie mambo ya ulimwengu.

Unatakiwa ama uwe umekufa kwa mambo ya ufalme wa Mungu na uwe hai kwa ulimwengu, au uwe hai kwenye ufalme wa Mungu na mfu kwa mambo ya ulimwengu. Huwezi kuwa hai kote kote.

**Maombi:** *Bwana, ninajua kwamba kukufuata wewe ndio kitu chenye usalama zaidi ulimwenguni. Nisaidie niwe mfu kwa ulimwengu na hai kwa ufalme wa Mungu.*

**Kwa usomaji zaidi:** ***Mathayo 19:16-22; Luka 12:32-34***

**Bado Anatenda Kazi Kwako.**

**Kifungu cha Kusoma: Wafilipi 1:3-14.**

*Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba Yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu.* ***Wafilipi 1:4-6***

Sunil ni mchoraji. Alipotaka kuchora picha alimwomba kijana mdogo akae kwenye kiti ili achore mchoro. Baada ya masaa machache, Yule kijana aliangalia kazi iliyofanyika na hakuweza kuelewa kile alichokuwa akifanya mchoraji. Alichoweza kuona ni alama kwenye turubai na akasikitika na kusema "Haa hii ni mbaya sana"Mchoraji akasema "Mwanangu tafadhali subiri, bado ninakushughulikia"

Nasi pia tunafanana na huyo kijana mdogo. Mungu anapoleta mambo yasiyopendeza maishani mwetu, mfano wa magonjwa, hasara, au hata maafa tunalalamika. Hatuoni lolote la maana katika hayo. Hata hivyo Mungu anacho kitu fulani chema katika mpango wake. Uwe na uhakika kuwa yeye aliyeanza kazi njema ndani yako ataikamilisha.

Paulo anaandika waraka huu akiwa gerezani huko Rumi. Je kifungo hiki cha Mmishonari mwaminifu wa Mungu sio kizuizi cha injili kusonga mbele? Kibinadamu, ndio! Hata hivyo, Paulo anasema ni mpango wa Mungu. "*.....lakini ndugu zangu nataka mjue ya kuwa mambo yote yaliyonipata yametoka zaidi kwa kueneza injili; hata vifungo vyangu vimekuwa dhahiri katika Kristo, miungoni mwa askari, na kwa wengine wote pia. Na wengi wa hao ndugu walio katika Bwana, hali wakipata kuthibitika kwa ajili ya kufungwa kwangu, wamezidi sana kuthubutu kulinena neno la Mungu pasipo hofu. Wafilipi 1:12-14.*

Sisi tu kazi ya mikono yake (Katika Kiyunani Poieema) (*Waefeso 2:10)*.ni sawa na kazi ya msusi. Msusi hufanya kazi kwa kutumia vifurushi vichache vya nyuzi. Lakini ana picha kamili mawazoni mwake. Sisi nasi ni kama hizo nyuzi. Hatakuacha ushindwe, bali ataimaliza kazi yake ndani yako. Mngoje kwa uvumilivu nawe utaona ni kwa jinsi gani atakavyofanya kila kitu kuwa chema kwa wakati wake.

*Ni Kitu kizuri; ni kitu chema*
*Yote yanayokutatiza anayaelewa anafahamu.*
*Unachotakiwa kumpa ni moyo wako uliopondeka na bila kusaza chochote.*
*Naye atafanya kitu kizuri sana ndani yako.*

***Maombi:*** *Bwana, nisaidie kungoja kwa uvumilivu ili nione kazi yako ndani yangu. Nina uhakika kwamba atakikamilisha kile alichokianza. AMEN*

***Kwa kujisomea zaidi: Waefeso 2:8-10; 1 Wakorintho 3:5-9.***

**Kutokupenda Maisha Yako**

**Kifungu cha kusoma: Ufunuo wa Yohana 12:7-12.**

*Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa.* ***Ufunuo 12:11***

Hapa, tunamwona shetani, mshitaki akiwa mbinguni. Kama ilivyokuwa kwa Ayubu, inawezekana alikuwa amewashitaki watakatifu kwa dhambi zao za zamani au kuhoji juu ya ukamilifu wao. Walishinda shitaka la kwanza kwa damu ya Mwana kondoo. Ushindi wa pili unathibitishwa kwa neno la ushuhuda wao. Wakisema " hatutarudi nyuma kwa kutokumfuata Bwana wetu hata kama itatugharimu kifo na maneno yao yakatibitishwa.

Wakati fulani mfalme mmoja alimwambia mtakatifu wa karne ya pili kuiacha imani yake vinginevyo mali zake zote angenyag'anywa. Mtakatifu akasema "Huwezi kufanya hivyo mfalme," " kwani akiba yangu yote iko mbinguni," mfalme akasema. "basi nitakupeleka mbali" Mtakatifu akasema" nipeleke mahali popote mfalme, Yesu wangu atakuwa nami" "sasa basi nitakuua" mfalme akaunguruma. "Lakini mfalme mimi ni mtu mfu tangu miaka arobaini iliyopita" ndiyo yaliyokuwa majibu ya mtakatifu.

Wale wasioogopa kifo hawaogopi chochote. Hawawezi kushawishiwa au kutishwa na chochote cha hapa duniani. Sio fedha, siyo kazi nzuri, wala maisha bora, vinavyoweza kukushawishi. Sio kutengwa, wala mashambulizi au chochote cha jinsi hiyo kinachoweza kukuogopesha kama tu hutayapenda maisha yako. Paulo anasema. "Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu kama kuumaliza mwendo wangu na huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu, kuishuhudia Habari njema ya Mungu" Matendo 20:24; matendo 21:13.

Kwa sababu hiyo basi, shetani hushindwa kabisa katika mashtaka yake na alitupwa kutoka mbinguni na Mikaeli na malaika zake. Hata hivyo, sio nguvu za malaika, lakini damu ya Mwana-Kondoo, na neno la ushuhuda ndivyo vilivyofanya ushindi upatikane. Hivyo Kama watakatifu wangeyapenda maisha yao, kuliko kujitoa kwao kwa Bwana wao, Malaika wasingeweza kumfukuza shetani. Tunapokuwa hatupendi kitu chochote, hata maisha na kumweka Yesu mbele, tunamshinda shetani.

**Maombi:** Ninaelewa kupenda maisha yangu ni mtego au kitanzi. Nataka kumshinda shetani kwa kukiri kwamba siyapendi maisha yangu. Kwa vyovyote vile nitakufuata wewe, Bwana wangu.

**Kwa usomaji Zaidi:** ***Matendo 20. 22-24; Luka 9.23-27; Matendo 15:26***

**Fikirini**

**Kifungu cha Kusoma: Wakolosai:3.1-17**

*Fundi saa alibainisha kwamba mtu mmoja alikuwa akija kila siku asubuhi na kurekebisha saa yake kulingana na saa kubwa ya ukutani iliyokuwepo dukani. Alipoulizwa, yule mtu alieleza akasema: "Mimi ndiye mpuliza king'ora hapa mjini na ninarekebisha saa yangu kutokana na saa yako kubwa na ninapuliza kinanda kulingana na saa yangu!"*

Fundi saa akaanza kucheka kwa sauti. Ha, ndugu! mimi ninarekebisha saa yangu baada ya kusikia king'ora, Akasema. Hatuwezi kurekebisha saa zetu kulingana na saa yoyote tu. Tunatakiwa turekebishe sawasawa na wakati unaokubalika. Kadhalika, hatuwezi kuruhusu fikra zetu kushawishiwa na mambo ya kipuuzi. Sisi sio wa ulimwengu huu, bali ni wa Kristo. (**Wakolosai 3.1**). Tunatakiwa tuweke mawazo yetu kulingana na viwango vya mbinguni Hatuishi kulingana na viwango vya ulimwengu. Watu wa ulimwengu huu watasema, hiyo ni kawaida, kila mtu anafanya hivyo. Inawezekana kila mtu anafanya hivyo, na hawaoni tatizo lolote. Hata hivyo, twaweza tu kufanya vitu ambavyo hata Yesu angeweza kufanya. Kwa hiyo, katika kila hali au jambo lolote, jiulize: "Je Yesu Angefanya Nini" (YAN)

Paulo hapa anatusihi sio tu kuwa makini na matendo yetu, lakini pia tusifikirie vitu ambavyo haviendani na Yesu. Wazo la kidunia litujiapo, akili zetu zisiliitikie. Kwa sababu wewe ni mfu, na maisha yako yamefichwa na Yesu ndani ya Mungu. Mtu aliyekufa hawezi kuitikia chochote! Unapopewa mapato ya udhalimu, ubinafsi, heshima isiyostahili, fikra zako haziwezi kupokea. Hiyo ni dhuluma ya asilia, kwa sababu fikra zako hazipo hapo.

Hata hivyo, uonapo mambo yanayoifurahisha mbingu, na kumpendeza Yesu, unajawa na furaha, kwa sababu fikra zako zipo katika mambo ya mbinguni.

***Maombi**: Bwana, sitazamii mapato ya vitu vya duniani, Ninajua, nimeitwa kuishi sawasawa na viwango vya mbinguni. Fikra zangu naziweka kwenye mambo ya mbinguni. AMINA*

**Kusoma zaidi:** ***Waebrania. 3:1; 11:13-16; 12:1-3***

Siku ya 8

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Shiriki Maisha, Sio Neno tu.**

**Kifungu cha Kusoma: 1 Wathesalonike 2:1-12**

*Vivyo hivyo nasi tukiwatumaini kwa upendo mwingi, tuliona furaha kuwapa, si Injili ya Mungu tu, bali na roho zetu pia, kwa sababu mmekuwa wapendwa wetu.* ***1 Wathesalonoke 2:8*** *Ilimpasa Paulo kuteseka sana huko Thesalonike. Lakini hilo halikuwa na umuhimu ukilinganisha na mateso yake pale filipi. (**1 Wathesalonike 2:2, Matendo 16:16-24**).*

Paulo aliweweza kutumia wiki tatu tu pale thesalonike na aliwapata Wayahudi wengi na Wayunani kwa Bwana. Hata hivyo, waongofu wapya walikuwa tayari kuhatarisha sana maisha kwa ajili ya Paulo huko Thesalonike.

Yason, aliyefungua milango ya nyumba yake kwa ajili ya wamishonari, alikokotwa na kuwekwa kifungoni kwa sababu aliwasaidia. (***Matendo 17. 5- 10***).

Msimamo wa Paulo ulikuwa nini alipokuwa Thesalonike?
Kifungu chetu kinasema vitu vingi. Wao (Paulo na Silas) walikuwa wakimpendeza Mungu, wakifanya kazi kwa bidii, kwa ungwana kama mama anyonyeshaye na upendo wa Baba! Hata hivyo, anasema hakuwepo pale kwa ajili tu ya kuhubiri injili, kupata roho na kujiachia! Kwa hakika alitaka kuona kuwa roho zinakombolewa. Lakini alifanya hivyo kwa sababu aliwapenda. Ukweli ni kwamba, alisema, hakutaka kuondoka Thesalonike kwa sababu ya mateso. Alihuzunishwa sana alipoona mamlaka zinamtesa Yason, aliyempatia mahali pa kuishi. Anasema, angeweza kutoa maisha yake hata kwa ajili ya Yason.

Siku za leo, tunasikia hadithi nyingi za mafanikio kutoka kwenye maeneo ya umisheni. Mamilioni wamesikia injili, maelfu wamempokea Yesu, mamia wamebatizwa na kadhalika. Vyema, lakini hebu fikiria, kwa nini tuhubiri injili. Paulo aliwapenda sana wale aliowahubiria injili, zaidi ya maisha yake.

Je tunao upendo wa namna hiyo kwa watu tunaowahudumia Ni nini kinatusukuma sisi kuhubiri injili? Je ni kwa ajili ya mzigo wa agizo kuu, au hamu ya upendo halisi tulionao kwa watu?
Kitu kimoja ni cha uhakika, tunashindwa mara nyingi kwa sababu tumeshindwa kuwapenda watu zaidi ya maisha yetu. Kumbuka kuwa, kama haumpendi mtu, huna haki ya kumhubiri injili.

***Maombi:*** *Bwana, mara nyingi upendo kwa watu umekuwa sio motisha yangu katika kuhubiri injili. Nisaidie kuelewa kuwa ninafanyika kuwa mwanafunzi wako pale tu ninapopenda. AMINA.*

**Kwa usomaji zaidi: *Matendo 16. 16-22; Matendo 17. 1- 10***

Siku ya 9

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Kuukomboa Wakati.**

**Kifungu cha kusoma: *Wakolosai 4:2-6***

*Enendeni kwa hekima mbele yao walio nje, mkiukoboa wakati. Ni nini kilicho zawadi ya thamani sana ya Mungu, nje yaYesu? bila shaka ni wakati! Pesa, zikipotea leo, zaweza kupatikana kesho. Kitu kingine chochote chaweza kupatikana tena, sio wakati*

Tumepewa wakati usiobadilika, unaolingana na umri wa maisha yako. Kwa hiyo, kutumia wakati maana yake ni kutumia maisha. Hupaswi kuupoteza wakati kwa uzembe au menejimenti mbaya. Ni lazima tuukomboe wakati! Paulo anatuambia tudumu zaidi katika maombi, tukikesha kwa kuomba pamoja na shukrani. **(mst.2)**

Wakati katika ulimwengu huu, tunapata zaidi kutokana na wakati tunaoutumia mbele za Bwana Mungu. Wakati unapokuwa unatumiwa kwa mazungumzo ya kipuuzi, masengenyo, kutazama vitu visivyokuwa vya maana kwenye runinga au kutafuta mitandao isiyo ya maana kwenye intaneti, tunapoteza wakati ambao tungeutumia kwa ajili ya Bwana. Hivyo tunaupoteza milele.

Njia nyingine tuwezayo kukomboa wakati kwayo ni kutumia wakati kwa kuwasaidia watu wapweke na waliokataliwa. Dini iliyosafi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, kwenda kuwatazama yatima, na wajane katika dhiki yao. ***Yakobo 1:27.*** Wanachohitaji zaidi sio fedha zetu, bali ni wakati wetu wa kuwa pamoja nao. Kuwatembelea yatima na wajane katika dhiki zao kunahitaji wakati. Lakini Mungu anaheshimu sana hilo. Amhurumiaye maskini, humkopesha BWANA, naye atamlipa kwa tendo lake jema. ***Mithali 19:17***

Kwa hiyo, kuukomboa wakati maana yake ni kuutumia mbele za Mungu, na kuutoa kwa ajili ya wahitaji na maskini. Wakati wa ziada, kama upo, ni lazima utumike kwa busara. Wenye hekima wataongea maneno ya neema tu yaliyokolea chumvi. (**mst 6**) Tunapotumia maneno makali au ya kuchukiza, watu huudhika. Baadae tena inatugharimu kwa kutafuta mapatano na kurudisha mahusiano. Kwa hiyo tusipokuwa na busara, hatupotezi tu wakati kupitia ugomvi na mashindano, pia wakati tunapoutumia kwa kutafuta mapatano.

***Maombi:*** *Yesu, nisaidie kutumia vizuri wakati wangu na wewe na kwa wanaoteseka. AMINA.*

**Kwa usomaji zaidi: Yohana *9:4-5; Mhubiri* 5.2-7**

Siku ya 10

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Mungu anapoanza kunitukuza**

**Kifungu cha kusoma:** ***Yoshua 3: 1-17***

*Bwana akamwambia Yoshua, hivi leo nitaanza kukutukuza mbele ya Israel wote, wapate kujua ya kwamba mimi nitakuwa pamoja na wewe, kama nilivyokuwa pamoja na Musa.* ***(Yoshua 3:7)***
*Musa aliyewaongoza watu wa Israel kwa miaka arobaini jangwani, sasa amekufa.* ***(Kumbukumbu 34:4-6)***

Yoshua akaagizwa na Mungu na kuteuliwa na Musa, kuwaongoza watu (wana wa Israeli) kuelekea kwenye nchi ya ahadi.(kumbukumbu 34:9-12). Alikuwa mwoga kiasi kwani alijua kuwa hakuwa kitu chochote akilinganishwa na Musa. Lakini Mungu akamtia moyo na kusema, Yoshua, kuanzia leo nitaanza kukutukuza, na Israel wote watajua ya kuwa niko pamoja nawe kama nilivyokuwa pamoja na Musa. Kumbuka, Mungu anamtukuza Yoshua, ili watu wajue kuwa yeye ana ushirika na yeye.
Tendo la kutukuzwa sio kuonyesha uko imara kiasi gani, ila kuthibitisha uwepo wa Mungu maishani mwako! Mtu mnyonge anapotukuzwa, wengine watajua kuwa kuna mtu aliye pamoja naye.

Mungu aliitimiza ahadi yake siku ileile. Mara tu nyayo za makuhani zilipokanyaga katika maji ya ukingoni mwa mto, ndipo maji yaliyoshuka kutoka juu yakasimama. Kama ilivyokuwa kwenye bahari ya shamu, watu wakapita kwenye nchi kavu. (***Yoshua 3:9-17***) Siku ile BWANA akamtukuza Yoshua mbele ya macho ya wana wa Israel; na wakamheshimu siku zote za maisha yake, kama walivyomheshimu Musa.**(Yoshua 4:14)** Hata hivyo, inawezekana kwamba Mungu anapotutukuza, tunajiinua. Tunaweza kudhania kwamba heshima tunayoipata ni majaliwa yetu (yaani tumejaliwa) au kipaji chetu.

Hadithi ya kufikirika inasema kwamba mwana punda ambaye alimbeba Yesu kuelekea Yerusalemu alikuwa anafurahisha na ni kwa uzuri au kupendeza kwa mwana punda ndio maana majoho yalitandazwa. Alipokuwa anarudi (mwanapunda) akaona dobi akitandaza majoho ili yakauke.

Mwanapunda akadhania yametandazwa kwa heshima yake, na kwa kujivunia akatembea juu ya yale mavazi. Hakuna haja ya kueleza alipigwa kiasi gani! Tunatukuzwa kwa sababu Yesu amepanda juu yetu (kama alivyopanda juu ya mwana punda). Ni Mungu aliye pamoja nasi ndiye anatutukuza. Watu wanapaswa kumuona Mungu na sio nafsi za watu.
Umetukuzwa sio kwa sababu wewe ni wakuu, lakini kwa sababu umembeba Mungu aliye mkuu.

**Maombi:** *Bwana, Ahsante kwa kunichagua kuwa pamoja nawe. Kila heshima na utukufu ni vyako, O Mungu, AMEN.*

**Kwa usomaji zaidi.** ***I Timotheo 1:15-17; Mathayo 5:14-16***

**Kuongozwa na Roho Na Kujaribiwa Na Ibilisi**

**Kifungu cha kusoma: *Mathayo 4:1-11***

*Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na shetani.* ***Mathayo 4:1***

Hii kwa sehemu inachanganya. Roho anamuongoza Yesu ili ajaribiwe na shetani. Kwa nini roho afanye hivyo? Mungu hatujaribu. “mtu ajaribiwapo, asiseme, Ninajaribiwa na Mungu, maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu.Yak 1:13 wakati mwingine hata hivyo huruhusu tujaribiwe. Wote tunaogopa majaribu.

Lakini kumbuka, majaribu ni fursa ya kuthibitisha ukamilifu wetu. Hii ni sawa na mtihani wa darasani. Kama hakuna mtihani unawezaje kupima uwezo wa mwanafunzi?. Hiyo ni sawa unaweza kusema, “lakini kibaya zaidi ni kwamba shetani ndiye anayetahini. Kwa nini asiwe malaika?”
Kwa swala la Ayubu, ukamilifu na wenye haki wake, shetani akasema, “Je! huyo Ayubu, yuamcha BWANA bure? ***Ayubu 1:9-10 .***
Shetani anapoleta chngamoto kama hiyo, Mungu anatupeleka kwenye mtihani, ambao unatungwa na shetani! Anasema, “Nenda, mwanangu! Chukua changamoto! Thibitisha uaminifu wako!”

Wakati mwingine watu huuliza, kwa nini Mungu aliweka mti wa mema na mabaya, ambapo alijua ungemshawishi mwanadamu. Kama Mungu asingeruhusu majaribu, Angekuwa kama Baba asiyempeleka mwanae kwenye mtihani, kwa kuogopa kwamba atashindwa.

Kwa nini Mungu hakuigilia kati wakati Hawa aliposhindwa?. Kama angefanya hivyo, angefanana na baba anayemfanyia mtoto wake mtihani!

Ni Mungu, ndiye alimweka Yusufu nyumbani kwa Potifa. Mungu aliruhusu hata mke wa Potifa, kubaki na kanzu ya Yusufu. Lakini Yusufu akatoka kwa ushindi kutoka kwenye vishawishi vya shetani. Akathibitisha usafi wake na ukamilifu wake. Mungu anataka tupitie majaribu na tushinde. Hapo ndipo, anaweza kusema kwa fahari, “ndio, utakatifu wa mwanagu umethibitika. Sasa, hakuna awezaye kumshtaki.”

**Maombi:** *Bwana, ninajua Hunijaribu ili nitende dhambi. Lakini, ukiniruhusu nipitie majaribu, nisaidie kushinda majaribu. Mimi ni dhaifu, bali wewe ni mwenye nguvu. Nipe nguvu. AMINA*

**Kwa usomaji zaidi: Mwanzo *39:1-23; Yakobo 1:12-15.***

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Toba Kutoka kwenye Kifo, kwenda kwa Mungu**

**Kifungu cha kusoma:** ***Matendo 20: 17-35***

*Nikiwashuhudia wayahudi na wayunani wamtubie Mungu, na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo.* ***Matendo 20: 21***

Neno "toba" lina maana zaidi kwenye Biblia kuliko linavyotumika kawaida. Katika maisha ya kale, tulimgeuzia Mungu migongo yetu, sio sura zetu. Tuliamini kwamba dunia, fedha, afya, mahusiano, marafiki na familia zetu zingetupatia yote tunayoyahitaji. Tulihangaika mchana na usiku kujipatia vitu na kudumisha mahusiano! Tulidhania dunia ni kila kitu, hivyo, tuliyatoa maisha yetu yote kwa tamaa za dunia.

Hata hivyo, mwishoni tukatambua kuwa mwelekeo haukuwa sahihi. Tulijutia maisha yaliyopita, ambayo hayakuwa na manufaa yoyote.ndipo ukaja ujumbe wa injili. Paulo anasema toba ni kuelekea kwa Mungu. Sio tu kuungama au kukiri dhambi zetu, au kuziombolezea. Inahitajika toba, kuachana na njia zetu za zamani, malengo na matakwa yetu na kumgeukia Mungu! Ni kuzitubia kazi zisizo kuwa na uhai. ***(Waebrania 6:1)*** na kutubu kwa Mungu! Sasa, njia yetu inakuwa Mungu, malengo yetu yanakuwa Mungu, na matakwa yetu yanakuwa Mungu! Hatuthubutu kutizama chochote-au hata kufikiri njia zetu na siku zetu za zamani, kwa msaada, hadhari au ulinzi na maongozi. Tunakuwa na lengo jipya, msaada mpya, na kituo kipya cha maongozi yaani Mungu!

Kwa nini tutubu kwa Mungu? Kwa sababu, tulianguka kutoka kwake! Tukianguka kutoka kwa Mungu, tunakuwa tumeanguka kutoka kwenye uzima. Baadae, matendo yetu yote yalikuwa matendo mafu.
Yesu alikuja hapa ulimwenguni ili kuturejesha kwenye uzima tuliopoteza, ili tuwe na huo uzima kisha tuwe nao tele. (***Yohana 10:10)***

Tunazitubia kazi zetu zisizo na uhai na kutubu kwa Mungu kwa ajili ya uzima. Tunapokea uzima, katika maana yake halisi ni katika uwepo wa Mungu, kwani kwake yeye ndimo ulimo uzima. **(Yohana 1:4)** Kwa hiyo, toba ni urejesho kwenye uwepo wa Mungu! Kama urejesho hautokei, toba haina maana.Tunapotubu kwa Mungu, tunaingia uzimani. Kila uzima lazima tuuishi, la sivyo hautakuwepo.Kuuishi uzima huo, tunahitaji imani ya Bwana wetu Yesu Kristo, anasema Paulo. Ndio maana alihubiri toba kwa Mungu na imani kwa Yesu Kristo! Hilo huifanya injili kukamilika.

**Maombi**: *Bwana, nazitubia kazi zilizokufa, na kutubu mbele zako. Wewe ndio lengo langu pekee, ni furaha yangu na mahali pa mwongozo wangu, AMINA.*

***Kwa usomaji zaidi: Matendo 2. 36- 41; Wakolosai 3. 5-14***

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Omba au Sifu, Lakini Kamwe Usiogope!**

**Kifungu cha Kusoma:** ***Yakobo 5:13-19***

*Mtu wa kwenu amepatikana na mabaya? na aombe. Ana moyo wa kuchangamka? Na aimbe zaburi.* ***Yakobo 5:13***

Inasemekana kuwa maisha ya mwanadamu ni mchanganyiko wa mateso na wingi wa utajiri? Wote tumo katika mojawapo ya hali hizo. Yakobo anasema, tunatakiwa kuomba tunapokuwa kwenye mateso na kusifu tunapobarikiwa. Hii ni mitazamo miwili tunayo takiwa kutunza.

Nyakati za mateso, tunaomba, lakini pia tunasumbuka au kuhangaika! Tunahangaika na kuomba. Maombi yetu mengi yanachipuka kutoka kwenye hofu na masumbufu. Hata hivyo, Mungu anatutaka tumtumaini na kuomba. Kumbuka, tumaini na wasiwasi haviendi pamoja. Ni maneno yanayopingana!( hofu na wasiwasi ni ndugu.) Kama unatumaini, huwezi kuwa na wasiwasi, na ukiwa na wasiwasi huwezi kutumaini. Unapokuwa na mateso na kama unamtumaini Mungu, ambaye anahusika na wewe ni nani anayeweza kukusaidia, maombi yako hayatachipuka kutokana na hofu au wasiwasi, bali kutokana na imani.

Tunafanya nini tunapokuwa tumebarikiwa? Yakobo anatuagiza tusifu! Sifa ni esemi wa hiari wa moyo wenye shukrani. Tunaomba tunapokuwa kwenye matatizo, tunasahau kutoa shukrani kwa Mungu tunapobarikiwa. Wana wa Israel walipokea mamia ya baraka walipokuwa jangwani.

Tunaona wanamsifu Bwana kando ya bahari ya shamu baada ya ukombozi wao kutoka kwa farao na Jeshi lake. Katika safari yao, walipitia matatizo mengi.Ingawa walishuhudia Jinsi Mungu alivyowajali na nguvu zake mara nyingi katika maisha yao, walinung'unika wakati wote, badala ya kuomba. Na Mungu alipowakomboa hawakumshukuru! Walikuwa ni watu wasio na shukrani. Tena, kusifu huelezea unyenyekevu.

Unapomsifu Mungu kwa baraka zake, unakiri kwamba haustahili kuzipokea. Unakuwa umempa Mungu kustahili kwake. Mtu mwombaji ni mnyenyekevu, kwani anakiri kwamba hawezi kukabiliana na hali yoyote mwenyewe. Mtu mwenye kusifu ni mnyenyekevu, kwani anakiri kwamba hastahili kile alichokipokea.

**Maombi:** *Bwana, nisamehe kwani nakuwa na wasiwasi kila wakati. Nipatie imani. Vivyo hivyo, nisaidie kuwa na shukrani, AMINA.*

**Kwa usomaji zaidi:** ***Wafilipi 4: 4-7; Mathayo 6:25- 34***

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Huko Nitakupa Pambaja Zangu!**

**Kifungu cha kusoma: *Wimbo ulio Bora 7: 9- 8:4***

*Huko Nitakupa Pambaja Zangu.* ***Wimbo ulio Bora 7:12***

Wimbo ulio bora umetafsiriwa katika njia nyingi tofauti. Ni kweli, inafafanua mtizamo wa kimwili wa upendo wa mme na mke. Hata hivyo maelezo yake mazuri yanapatikana inapoelezewa kama mahusiano ya upendo kati ya Kristo na kanisa lake. Katika kitabu hiki, tunamwona kijana mchungaji anayependwa na mshulami mpendwa wake. Vilevile, tunamwona mfalme katika mandhari, anayetaka kuvamia pendo la mshulami. Mfalme alimleta kwenye chumba chake na mabinti wa mjini (mabinti wa Yerusalemu) wanauelezea ukuu wa enzi ya mfalme na upendo wake. Hata mfalme anaeleza ni jinsi gani anampenda. Hata hivyo mshulami anatunza upendo wake kwa mpendwa wake.

Katika sura ya saba, mshulami ni mateka chumbani mwa mfalme. Aidha mabinti wa mjini, au mfalme mwenyewe anaelezea uzuri wake.(**mst 6-9)**
Lakini tafsiri za Biblia nyingi zinaugawanya ***mstari wa 9,*** hizi ni pamoja na NIV, NKJV and NASBU. Wanasema nusu ya mstari umesemwa na mfalme na nusu mshulami mwenyewe.

MFALME ANASEMA…9 na kinywa chako kama divai iliyo bora. MSHULAMI ANASEMA: kwa mpendwa wangu inashuka taratibu, ikitiririka midomoni mwao walalao. ***Mst 10,*** Mimi ni wake mpendwa wangu, na shauku yake ni juu yangu. Mshulami anasikia maelezo ya mfalme, lakini anasema, ": kwa mpendwa wangu inashuka taratibu, ikitiririka midomoni mwao walalao. Mimi ni wake mpendwa wangu, na shauku yake ni juu yangu!"

Wakati dunia inapojaribu kuharibu pendo letu, kumbuka, shauku ya mpendwa wako ni kwako! 'Njoo, mpendwa," anasema mshulami, "twende mashambani….huko nitakupa pambaja zangu." Anataka kuepukana na ubatili wa mjini. Moyo wake unatamani kuwa na mpenzi wake mashambani! "huko nitakupa pambaja zangu."

Wote tunapaswa kutunza aina hii ya kutoridhika kwa ajili ya tamasha ya ulimwengu wa kisasa. Ni kwenye faragha tu, tunapoweza kumwaga pendo letu kwa mpendwa wetu.

**Maombi:** *Bwana, nisaidie kutoridhika au nisiridhike na fahari zisizo na maana za ulimwengu huu. Naomba niwe peke yangu pamoja nawe, na ninataka kumwaga pendo langu kwako, AMINA.*

**Kwa usomaji zaidi: *Zaburi* 27:1-6; *Wafilipi* 3:7-11**

Siku ya 15

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Sauti ya Kipekee!**

Kifungu cha Kusoma: 2 Nyakati 18:1-34

*Mikaya akasema, kama aishivyo BWANA, neno lile atakalolinena Mungu wangu, ndilo nitakalolinena. 2 Nyakati 18:13Yehoshafati, mfalme wa Yuda, alifanya ujamaa na Ahabu, mfalme wa Israel.Ahabu alitaka yehoshafati aende naye vitani dhidi ya washamu. Alikuwa tayari kwenda lakini, kwa kumwogopa Mungu, akasema, ni baada ya ridhaa ya Mungu!" njia rahisi ilikuwa ni kumuuliza nabii. "hilo sio tatizo", Ahabu akasema" ninao 400 himaya yangu."*

"kwea, kwa kuwa Mungu atautia mkononi mwa mfalme," manabii wote wakasema! Yehoshafati, hata hivyo, hakuwaamini. "Je hayupo hapa nabii wa BWANA tena, ili tumuulize yeye? Akauliza. "Yupo mtu mmoja, ambaye tungeweza kumwuliza BWANA kwa yeye, lakini namchukia; kwa sababu hanibashiriimema kamwe" ahabu akasema. Ni huzuni ilyoje? Mfalme alitarajia nabii kuruhusu tamaa zake zote mbaya.Nabii mikaya, muasi machoni pa Ahabu, mwishowe akaulizwa. Mikaya akasema, kama aishivyo BWANA, neno lile atakalolinena Mungu wangu, ndilo nitakalolinena.

Kwa nini Mikaya! Kwa nini usiwe kati ya 400 wengine? Mjumbe wa mfalme akamuuliza akisema, " angalia maneno ya manabii kwa nia moja yasema mema kwa mfalme, neno lako basi na liwe kama mojawapo lao, ukaseme mema. Anaongea kwa niaba ya Mungu! Ni nani anayeamua yaliyomo kwenye ujumbe? Sio mjumbe, wala anayepelekewa ujumbe. Ni mwenye ujumbe.... Mungu mwenyewe!

Sauti ya Mikaya ilikuwa ni sauti ya kipekee. Hakuwa tayari kuchukuliana na uovu. Hata hivyo, palikuwepo manabii 400, waliotabiri "kwa jina la Bwana" (mst 10) na walikuwa tayari kufanya maafikiano.

"oh Micah, anatabiri iliyo kweli. Je tuende Ramoth-gileadi vitani? Mfalme akauliza. Manabii wako kiofisi walisema nini? Kwa nini usisikilize sauti yao na ukwee? Mikaya akamdhihaki mfalme. "Walichokisema ni kweli yao au kweli yako. Lakini nakwambia "iliyo" kweli. Israel watakuwa kama kondoo wasio na mchungaji. Uko tayari kwenda na kufa vitani."

Mikaya akatupwa gerezani kwa maneno yake ya kutokuchukuliana na uovu, lakini alichokiongea ulikuwa ukweli wa Mungu. Mfalme Ahabu akafa kama iivyotabiriwa.

**Maombi:** *Bwana nisaidie nisimame kutobadilisha kweli yako, hata inaponipasa kuteseka kwa ajili yake.*

**Kwa usomaji zaidi: Mika 2: 6-11**

**Kiandike hicho juu Yangu.**

**Kifungu cha kusoma:** *Filemoni 1:1-25*

*Na kama amekudhulumu, au unamwia kitu, ukiandike hicho juu yangu.*
***Filemoni 1:18***

Watu sio roho. Wana utu na mahusiano ya kijamii.

Paulo, akiwa gerezani, akawa baba wa kiroho wa Onesmo, mtumwa aliyetoroka.(hata gerezani panawezakuwa mahali pa uinjilisti. Onesmo sasa anamtumikia Paulo gerezani. Alikuwa ni mtu sahihi, anayefaa na alitumika (hiyo ndiyo maana ya jina lake –**mst 11**) Paulo alimwona kama moyo wake mwenyewe (**mst. 12**) Paulo alifurahia kumteua kama msaidizi wake (**mst 13**)

Hata hivyo, alitaka kumpeleka mwongofu wake mpya kwa Bwana wake. “ lakini sitakutaka kutenda neno lolote isipokuwa kwa shauri lako, ili kwamba wema wako usiwe kama kwa lazima, bali kwa hiari.”(mst14) Angalia ni kwa namna gani Paulo anavyomshughulikia mwongofu wake.
Alipomrudisha, alimtambulisha Onesmo kama mwanae, sio kama aliyekuwa mtumwa wa Filemon, au sio hata kama “ndugu wa Onesmo” (kama Filemon angemtazama kama aliyekuwa mtumwa wake, angemtizama kwa kinyongo lakini Sasa, Onesmo ni mtoto wa Paulo!). “Na kama amekudhulumu, au unamwia kitu, ukiandike hicho juu yangu. Mimi Paulo nimeandika kwa mkono wangu mwenyewe, mimi nitalipa” (**mist 18-19**)

Paulo alikuwa tayari kulipa gharama ya mtu aliyempokea Yesu. Hakuwa kama mafarisayo aliowaongelea Yesu kwenye kitabu cha **Mathayo 23:15** “ole wenu waandishi na mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnazunguka katika bahari na nchi kavu ili kumfanya mtu mmoja kuwa mwongofu, na akiisha kufanyika, mnamfanya kuwa mwana wa jehanam mara mbili zaidi kuliko ninyi wenyewe. Uinjilisti ni kutoa. Unakuhitaji wewe na vile ulivyonavyo.

Wote tunaongea kuhusu Yohana 3:16-”upendo mkuu” Mungu aliouonyesha kwa mwanadamu. Vipi kuhusu 1 Yohana 3:16? “Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu.” Ukimwona mtu asiyekuwa na msaada, je unaweza kusema, “kiandike hicho juu yangu.

**Maombi:** *Bwana, nisaidie kuelewa kwamba kushuhudia ni kutoa, AMINA.*

**Kwa usomaji zaidi: Yakobo 2:8-20, 1 Yohana 3:16-20**

Siku ya 17

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Maata: Je ni lugha ya Mungu?**

**Kifungu cha kusoma:** ***Yoel 1:1-20***

*"…..nzige na parare, na madumadu, na tunutu, jeshi langu kubwa nililotuma kati yenu."* ***Yoeli 2:25***

Kuna kitu kibaya sana kilitokea katika maisha ya wana wa Israeli, ambacho hakikuwahi kutokea katika siku zao, au katika siku za baba zao! " yaliyosazwa na tunutu yameliwa na nzige; yaliyosazwa na nzige yameliwa na parare; yaliyosazwa na parare; yameliwa na madumadu" ( **Yoeli 1:4; 1:2-5**).
Nani yupo nyuma ya hili? Shetani, yule adui? Kwa mshangao, Mungu akatamka kwamba alihusika katika janga hilo. " nzige walikuwa jeshi langu, "akasema Mungu! Nilisema nanyi….lakini hamkunisikia." Mara nyingi majanga yanatoka kwa Mungu, japo tumeshidwa kuitambua kuwa ni lugha ya Mungu.

Nyumba iliyojengwa kilimani peke yake iliungua moto. Watu walipoona wakiwa mbali, walikimbia kwenda mahali pale. Mlango wa kuingilia ulikuwa wazi. Wakavuta na kutoa vitu vyote vya thamani nje ya nyumba na, kwa mshangao, wakakuta chumba cha ndani kimefungwa na kufuli kwa ndani na wanafamilia walikuwemo ndani wakitazama televisheni.

Walipotoka nje ya chumba na kuona vitu vyote vya thamani vimetupwa nje, wakapiga kelele: "ni nani aliyewapa mamlaka ya kutupa thamani zetu nje?" Mtu mmoja akawaonyesha moto na kusema, "haikuwa shauku yetu kufanya hivyo ndugu, ila nyumba yako ilikuwa inaungua."

Levukeni, enyi walevi, mkalie; asema Bwana.( Yoeli 1:5) kwa nini hata haulii? Umelewa? Amka! Watu wanalewa na pesa, cheo, falsafa, majivuno… wanashindwa kusoma lugha ya Mungu! Majanga kwao yamekuwa ya asili au kawaida! Mungu asema… Mimi Ndiye nimeleta janga hili.

Mimi ndiye nimetoa thamani zako zote. Tunalia…. Kwa nini Mungu? Kwa nini unanivunja? Kwa nini unachukua vitu vyangu? Jibu ni rahisi…. Unaelekea kwenye moto wa milele!

Mungu anatuma nzige, "Jeshi lake kubwa ili" kukufundisha somo.Anaruhusu majanga maishani mwako ili kukuokoa usiingie kwenye majanga makubwa ni vyema ujifunze somo mapema.
Hivyo anza kuona matukio maishani mwako kama Lugha ya Mungu. Yaitikie kiroho.

**Maombi:** *Nisaidie Bwana kuelewa lugha yako. Nisafishe kupitia kwenye kazi yako ndani yangu.*

**Kwa usomaji zaidi: Isaya 59:9-11; Kumbukumbu 28:1-29**

**Tafuta Maskani Ndani ya Yesu**

**Kifungu cha kusoma: Yohana 14:1-27**

*"Nyumbani mwa Baba yangu mna Makao mengi…."* ***Yohana 14:2***

Mtu wa kale aliishi kwenye Mapango. Mtu wa sasa ana nyumba za starehe na hata majumba makubwa.

Hata hivyo, wanashindwa kupata chumba au nafasi kwa ajili ya masumbufu ya mioyo yao.Yesu akasema, "msifadhaike mioyoni mwenu, mnamwaminini Mungu; niamininini na Mimi." Yohana 14:1 Hakuna mjuaji na mkuu awezaye kuja na kukufariji namna hii. Unahitaji sababu ya kuondoa woga wako. Yesu anakupatia sababu. "Kumtumaini Mungu na kunitumaini mimi kutatatua maswali yako" ni Yesu pekee anayeweza kusema hayo. Kutumaini ni kutegemea kwa vyote. Fikiria umezimia na unataka kuanguka, unajiegesha.

Sasa, haujasimama peke yako… Hauwezi! Umepoteza nguvu zako zote. Unaweka uzito wako juu ya mtu uliyemuegemea… hilo ndilo "tumaini." Kama unamtumaini Mungu, Yesu, kwa jinsi hiyo, hutapaswa kusumbuka, kamwe! Kwa nini watu maarufu wanajinyonga hata baada ya kumiliki majumba ya kifahari kila bara? Tumaini lao liko kwenye fedha na umaarufu, lakini vitu hivyo vya kuharibika, haviwezi kubeba mizigo yao. Vitu vyao vyote vya ghali, mavazi mazuri hayatoshi kupangusa machozi ya ndani ya mioyo yao inayosumbuka. Wanajaribu kuwaegemea marafiki zao, lakini wao pia ni kama "kuta zilizoinama."(Zaburi 62:3) zinaanguka! Oh! Ebo Na wamwegemee Yesu, mwamba wa milele, anayeweza kubeba mizigo!

Yesu anaandaa makao kwa ajili yako mbinguni;lakini unapaswa kutafuta makao ndani yake hapa duniani. Yesu anakutaka ukae ndani Yake! (Yohana 15:4) Hapo sasa makao ya milele ambayo Yesu anaandaa yatakuwa yako. Kukaa sio kutembelea. Kukaa ni kubakia hapo au humo. Ni sawa na tawi likaalo kwenye mzabibu. Katika shughuli za masaa 24 na siku 7 za wiki.
Mfanye Yesu kuwa makao yako ya kudumu. ukifanya pumziko kwa kitu chochote au mtu yeyote zaidi.

Ukipata makao ndani ya Yesu, na ndani yake tu hapa duniani, kamwe hatakuacha mkiwa. Atarudi tena na kukuchukua pamoja nae, ili kwamba alipo yeye na wewe uwepo." Ukijitenga pekee yako na kuwa kwenye mikono ya Bwana, na yeye hatakutelekeza mikononi mwa mtu yeyote.

**Maombi:** *Bwana, mimi nimechoka. Ninakuegemea wewe. Najua nipo kwenye mikono yako salama. AMINA.*

**Kwa usomaji zaidi: Zaburi 23:1-6, Yohana 16: 16-24**

## Na Iwe Nuru

**Kifungu Cha Kusoma: Mwanzo 1:2-4**

*" Na Mungu akasema, "Iwe nuru" ; Ikawa nuru."* **Mwanzo 1:3**

Mungu akaona, kuwa dunia aliyoiumba ilikuwa ukiwa na utupu. Mungu akashuka ili kuona kilichotokea. Kila kitu kilikuwa hakieleweki kwa sababu giza lilikuwa juu ya vilindi vya maji! Nani aliumba giza?

Hakuna haja ya kuumba giza….ondoa nuru na tayari kutakuwa na giza. Giza sio kitu kilichopo. Ni kutokuwepo kwa nuru. Palitokea, wakati kulikuwa na sherehe ya usiku, mtu mzima mmoja alitoa taa yenye nuru na akamwambia kijana aiweke mahali popote atakapokuta giza. Baada ya kijana kutembeatembea kwa mda, akasema hakuweza kuona giza! Ndio kwa, maana popote kijana alipopeleka taa yenye nuru, giza lilikimbia na nuru ikatawala! Pasipo na nuru, ni giza. Palipo na nuru, giza halipo. Ni vitu viwili visivyoendana.

Giza liliigeuza dunia kuwa utupu. Kwa kweli, tatizo halikuwa giza, ila ukosefu wa nuru. Kuijenga tena dunia, nuru ni lazima irudi! Kwa hiyo, Mungu akasema-iwe nuru, na ikawa nuru! Na nuru ikaleta uzima, na, uzima ukaleta kila kitu. Haichanganyi kuona kwamba nuru iliumbwa siku ya kwanza, huku Mungu aliumba jua siku ya nne?

Katika ufafanuzi wa uumbaji, si giza wala nuru vinavyorejewa hasa. Katika muktadha huu, giza ni giza la kiroho. Dunia haikuwa na Mungu, na ikawa ukiwa. Giza lilikuwa juu ya vilindi, kwa sababu hapakuwa na nuru, au kwa lugha nyingine, kwa kukosa uwepo wa Mungu! Kuweka mambo sawa, nuru ya jua haukuhitajika, bali nuru ya Mungu…..kwa hiyo, Mungu alituma nuru yake ulimwenguni, na ulimwengu ukajengwa upya! "Ndani yake ndimo ulimwokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu" Yohana 1:4 Jua sio chanzo cha nuru. Mwana ndiye.

Ni Mungu! Yeye mwenyewe ni nuru, wala giza lolote halimo ndani yake! (1 Yohana 1:5) katika uwepo wake, kila kitu ni nuru. Pasipo yeye, kila kitu ni giza. Mungu alituumba kama wana wa nuru. Sisi, hata hivyo, tulijitoa gizani mara nyingi zaidi. Tunamhitaji Mungu atuatamie juu yetu ili kwamba giza ndani yetuligeuzwe kuwa nuru.

**Maombi:** "*niangazie, ee Mungu Mtakatifu, ili niweze kuangaza nuru yako.*

**Usomaji zaidi: Yohana 1:1-1, 1 Yohana 1:5-7**

**Tuwe Hodari!**

**Kifungu cha kusoma. Kutoka 1:1-20.**

*Wanawake wa Kiebrania si kama wanawake wa Kimisri; kwa kuwa ni hodari nao huzaa kabla mzalisha hajapata kuwafikiria"* ***Kutoka 1: 19***
*Waisraeli walienda Misri " wakiwa wachache" (* ***Kumbukumbu 26:5****), lakini sasa "wameongezeka mno" (****Kutoka 1:7****). Adui aliogopa! (kutoka 1:12) Hivyo walipanga kufanya uharibifu. (****mst 10****)*

Adui aliwakandamiza ili kuwapunguza idadi. Lakini jinsi walivyokandamizwa zaidi, ndivyo walivyoongezeka! Farao, mfalme wa misri, aliwaagiza wazalishaji kuua kila mtoto wa kiume wakati wa kuzaliwa.

Wazalishaji walikuwa wakimcha Mungu! ( Farao aliwaogopa Waisrael, lakini wazalishaji walimcha Mungu! Mungu akawapa familia(mst 21) Farao hakumcha Mungu hivyo Mungu aliondoa familia yake-wazaliwa wa kwanza.) Adui hatafuti vita ya wazi. Anatenda kazi kiuerevu. (**mst 10**) Shetani ni mwenye hila. Zijueni hila zake.(**Efeso 6:11**). Adui hataki kuona uzao mpya ukitokea kati ya wana wa Mungu. Atafanya hila zake zote kuhuzunisha wazaliwa wapya. Hata hivyo, wanawake wa Israel walikuwa hodari na walijifungua hata bila msaada wa mzalishaji. (**mst 19**)Israel ya zamani ni alama ya kanisa jipya. Adui hataki kuona uzao wowote mpya ukitokea kwenye ufalme wa Mungu.

Hata hivyo, Mungu anataka kuliona kanisa Lake linakuwa hodari katika kuzaa. Anatarajia watoto imara, ambao wataweza kuangusha ngome ya shetani wazaliwe. Lakini tunaona nini kwenye makanisa ya leo? tunatoa sauti za kuelemewa wakati wa uchungu wa kuzaa, lakini hakuna mtoto.
Tuna uchungu wa kuzaa, lakini hatuzai. Mara nyingi wazalishaji-sio Wamisri bali Waisrael, wanawaua watoto wa kiume. Tumepoteza uhodari wetu! Tumepoteza hata hamu yetu ya kuzaa.

Wengine hudhani uzazi wa mpango unahitajika makanisani.Tumeridhika na idadi yetu. Kwa waliowengi, wazawa wapya ni chanzo cha usumbufu! Tunasahau ukweli kuwa tuko vitani. Wengi wetu tunauona ulimwengu kama sio adui yetu, bali kama rafiki asiyeeleweka! Badala ya kupigana tunatafuta muafaka…..

Kumbuka, adui haogopi kanisa linalofanya muafaka na ulimwengu. Lakini anatetemeka aonapo kanisa hodari likizaa watoto imara!

***Maombi****: Bwana, naomba mimi na kanisa langu tuwe hodari katika kuzaa watoto wa kiroho. Tusaidie kuharibu milango ya kuzimu-Amina.*

**Kwa usomaji zaidi: Matendo 8: 1-8, Ufunuo 7: 9-17**

**Kukesha, hata wakati wa raha.**

**Kifungu cha kusoma: Waamuzi 7:1-8**

*"Kwa watu hawa mia tatu walioyaramba maji nitawaokoa, nami nitawatia Wamidiani katika mikono yako"* ***Waamuzi 7:7-8***

Gideoni Alipoita watu kwenda vitani, waliojipanga kwenye mstari walikuwa 32,000 wenye nguvu! Lakini Jeshi la adui lilikuwa kubwa, kama kundi la nzige; na ngamia wao walikuwa hawahesabiki" Waamuzi 7:12. Gideoni alifikiri anahitaji watu zaidi kupigana, lakini Mungu akamwambia jeshi alilonalo ni kubwa mno, "anayeogopa na kutetemeka na arudi nyumbani," Gideoni akatangaza. Watu ishirini na mbili elfu wakaondoka, na kumi elfu wakabaki. Waoga hawana nafasi kwenye Jeshi la Mungu!

Gideoni inawezekana alikerwa kuona watu walivyorudi nyuma. Angeweza kufanya nini na elfu kumi tu, wakati jeshi la adui ni kama mchanga kwenye ufukwe wa bahari! Lakini, Mungu akasema idadi bado ni kubwa mno. Mchujo mwingine ulihitajika. Gideoni akawaleta watu chini majini, ili wanywe! Watu mia tatu wakanywa maji kwa kurambaramba kama mbwa.

Wengine wote wakapiga magoti na kunywa. Bwana akamwambia Gideoni, "Kwa watu hawa mia tatu walioyaramba maji nitawaokoa, nami nitawatia Wamidiani katika mikono yako" Kwa nini wale walioyaramba maji kwa ulimi walionekana wanastahili kwenda vitani na waliokaa chini hawakustahili?

Mwangalie mbwa! Macho yake huwa yamefunguliwa wakati anapokunywa maji. (sio kama paka anywapo maziwa). Hayaangalii maji ila anatazama kila upanda. Mbwa anakesha hata pale anapokunywa maji.

Wale walioyaramba maji kwa ulimi wao wanakesha hata wakati wa raha. Wana kitu kimoja tu machoni pao-VITA! Tuko vitani dhidi ya adui yetu, shetani. Wale wanaokaa chini, maji ndiyo yalikuwa kipaumbele chao, sio vita.
Mungu hataki tusahau wito au ujumbe wetu tunapokuwa kwenye faraja. Unahitaji kunywa maji, ila wewe usinywewe na maji. Tazama, hawa watu 9,700 walikataliwa na Bwana hawakuwa waoga (hawakuliacha jeshi waoga walipoambiwa waondoke) ila hawakukesha. Mungu hataki tu tusiwe waoga bali tukeshe au tuwe waangalifu.

**Maombi:** *Bwana, sitaki kuliwa na raha. Nisaidie kuona. Nisaidie kuona hatima ya ufalme wako machoni pako! AMINA*

**Kwa usomaji zaidi: 1 Peter 5:6-11; 1 Korintho 7: 28-31**

Siku ya 22

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Shuhudia Tabia Yako**

**Kifungu cha Kusoma: Mwanzo 5:19-23**

*"Kwa imani Henoko alihamishwa, asije akaona mauti, wala hakuonekana, kwa sababu Mungu alimhamisha; maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu."* ***Waebrania 11:5***

Kwa kawaida tunanena mema kwa wale waliotutangulia. Ilitokea, kijana mchafu, fidhuli na muovu akafa. Kwa kutotaka kuumiza mioyo ya wafiwa kwa kusema "kweli", kila mtu msibani alimsifu aliyekufa kwa kusema alikuwa mkarimu na mwenye huruma. Aliposikia tathmini za uongo, mjane wa marehemu akamwita kijana wake na kumwambia; "mwanangu,umesikia yaliyosemwa kumhusu baba yako? Nenda kwenye jeneza, chunguza kwa karibu kuhakikisha kama ni Baba yako kiukweli."

Kama ukiishi maisha mazuri, watu watakusifu utakapokufa. Hata hivyo, Ushuhuda halisi unaoupata kuhusu maisha, sio wakati wa kufa bali hata wakati ukiwa hai. Henoko aliishi kwa imani. Hili lina maana gani? Aliishi maisha ya kujitoa kikamilifu kwa Mungu. Wakati wote alimpendeza Mungu. Kwa namna Fulani, alitaka kuleta tabasamu usoni kwa Mungu. Siku zote alitafuta mapenzi ya Mungu na kuyatii.

Alimpendeza Mungu kwa kujiweka katika hali ya utakatifu ili kutembea na Mungu mtakatifu. Hii haimaanishi kuwa kila mmoja alipendezwa na Henoko. Nina uhakika kuwa Henoko hakuwapendeza wengi walioishi nae wakati ule. Huwezi kumpendeza Mungu na wanadamu kwa wakati mmoja. ('Wanadamu' hapa maana yake watu wenye ufahamu wa kidunia)

Hata hivyo, watu ambao hawakumthamini walimshuhudia kwa jambo moja kutoka mioyoni mwao: "mtu huyu alikuwa na jambo moja tu…. Kumpendeza Mungu wake."Labda watu wa wakati wake walimdhania Henoko ana wazimu, asiyefaa kwa maisha ya ulimwengu….Ndiyo! labda ndio sababu Mungu alisema, "njoo kijana, nitakuweka mahali unapostahili!"
Je ungependa kuishi maisha yatakayofanya uso wa Mungu uwe na furaha? Hilo litakugharimu, ila bora hilo.

Je watu wanaokuzunguka…familia yako, marafiki, majirani, washirika, na wasafiri wenzako ndani ya reli za chini ya ardhi, wauzaji wa maduka ya bidhaa ndogondogo….watashuhudia maisha yako kama yanayompendeza Mungu wako tu?

**Maombi:** *Bwana, nisaidie nisababishe uso wako utabasamu, Amina!*

**Kwa Usomaji Zaidi: Ayubu. 1: 1-8; Luka 7. 2-11**

**Mkiri yeye Mbele za Watu**

**Kifungu cha Kusoma: Luka 12:1-12**

*"Nami nawaambia, kila atakayenikiri mbele ya watu, Mwana wa Adamu naye atamkiri yeye mbele ya malaika wa Mungu. Na mwenye kunikana mbele ya watu, huyo atakanwa mbele ya malaika wa Mungu.* ***Luka 12:8-9***

Mtu wa leo anamtamani Yesu, lakini ni mara chache anakuwa amemkiri Yeye. Wakati mwingine watu husema... "Nampenda Yesu. Anaujua moyo wangu. Nitatunza dini yangu kwa ajili yangu. Kuna haja gani ya kumweleza kila mtu?" lakini rafiki, kama moyo wako umejawa na Pendo la Yesu, ni nini kinakuzuia usimwage upendo huo mbele za watu? Ni woga, sawa? Unawaogopa watu.

Yesu ni Bwana harusi wetu. Hakuna bibi harusi anayesita kumkiri bwana harusi mbele za watu. Bali,atafanya hivyo kwa kujiamini. Kuna nini cha kuonea aibu, unaposema kwa watu kwamba wewe ni Bwana harusi wa Yesu na Yeye ni mwokozi, Bwana, na Mungu wa milele? Kumbuka, mamilioni wamejitoa mhanga kwa kukiri imani zao. Unadhani ukiri wao ulikuwa upumbavu?

Siku za leo, hata waenda kanisani wanaogopa kumshuhudia Yesu. Imani yao haijulikani kwa wale walionao mashuleni, maofisini, na mahali pa kazi. Wanaabudu ndani ya kanisa, ila wanaogopa au wanaona aibu kukiri mbele za watu. Unahitaji kuikiri imani yako "mbele za watu" sio kanisani tu. Kama unaona aibu, Yesu anasema, itampasa "akukane wewe mbele ya malaika wa Mungu!"

Unamwogopa nani? Yesu akasema; "msiwaogope hao wauuao mwili na baada ya hapo hawana wawezalo kutenda zaidi. Lakini nitawaonyesha mtakayemwogopa; mwogopeni yule ambaye akiisha kumwua mtu ana uwezo wa kumtupa katika Jehanamu; naam, nawaambieni mwogopeni huyo." ( **Luka 12:4-5**). Mwogopeni Mungu! Unajua ni nini kilicho mbele ya wale wanaomkana Mungu na kupokea alama ya mnyama?....naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za mwana kondoo. ( **Ufunuo 14:10**)

Hebu na tujivunie kumshuhudia Yesu mbele za watu. Unajua thawabu yake? Yesu atatukiri mbele za malaika.... Kwa ujasiri atasema nao, "tazama, bibi harusi wangu aliyenipenda zaidi na kunikiri mimi mbele za watu bila woga na aibu!" tunahitaji nini zaidi ya hicho mbinguni?

**Maombi:** *Bwana, nisaidie nisiwe na aibu na woga kuuambia ulimwengu kwamba mimi ni wako, AMINA!*

**Kwa usomaji zaidi**: I Petro 4. 12- 19; 2 Timotheo 2 8-11; Ufunuo 12. 7-12

**Mungu Aliwachagua Waliodhaifu.**

**Kifungu cha Kusoma: 1 Korintho 1: 16-31**
*"Bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia ili awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu.* ***1 Korintho 1:27***

Wengi walio na hekima ya ulimwengu hawachagui maisha ya Imani. Wanafikiri wanaweza wao wenyewe. Wanafikiri ni "upumbavu" kuacha hekima yao na kufuata maisha "yasiyo na uhakika". Paulo anasema Mungu aliwachagua "wapumbavu" kuwaaibisha wenye hekima. 'Wenye hekima kutokumchagua Mungu ni upande mmoja wa hadithi. Ukweli ni kwamba Mungu hakuwachagua wenye hekima wa dunia hii!

**Luka 19:28-40**, inaongelea kuhusu "mwana punda aliyefungwa" kabla ya kusulubishwa, Yesu alitakiwa kuingia Yerusalemu, jiji la Mfalme. Yeye ni mwana wa Daudi, mfalme wa milele! Sasa ni wakati wa mfalme wa wafalme kuwa na mwendelezo wa Ufalme. Alihitaji chombo cha kumbeba. Ni mnyama gani ambaye angefaa? Tembo, kama ilivyokuwa kwa mfalme wa mashariki? Au, farasi kama ilivyo kwa mfalme wa magharibi? Au, angalau ngamia kama ilivyokuwa kwa mfalme wa jangwani?

Hapana! Mungu aliamua kupanda mwanapunda! Akawaambia wanafunzi wake waende kijiji kilichoko mbele yao, ambapo watamwona mwanapunda amefungwa, ambaye hakuna aliyewahi kumpanda…..hatujui ni kwa nini. Labda hakuna aliyetaka kumpanda.

Kwa dakika, mwanapunda ambaye hakuwahi kupandwa, akawa "mwanapunda wa kifalme" Kila mtu akaanza kutandika nguo njiani. Ndiyo ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana ambaye amemkalia. Kulingana na Paulo, Mungu alimchagua mwanapunda kumuaibisha Ndugu Tembo, na Mheshimiwa Farasi na Daktari Ngamia! Walidhania wanastahili kumbeba "Mtukufu", lakini Mungu hakuona kama wanastahili kumbeba. Hisia zao za "kustahili" zilikuwa ni kutokustahili, na hisia za mwanapunda za "kutokustahili" zikawa kustahili.

**Maombi:** *Bwana, ninajua kuwa mimi ni kiumbe kisichostahili! Ulinichagua bila sababu, ila kwa rehema zako. Hebu na nijisifu kwa ajili yako, na wewe peke yako, Bwana wangu! AMINA.*

**Kwa Usomaji Zaidi: Luka 7: 36-50; Marko 11:1-11**

Siku ya 25

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Nitawezaje?**

**Kifungu cha kusoma: 2 Samuel 11. 1- 17**

*"Sanduku na Israel na Yuda, wanakaa vibandani; na Bwana wangu Yoabu, na watumishi wa Bwana wangu, wamepiga kambi waziwazi uwandani; nami niende nyumbani kwangu, kula na kunywa, na kulala na mke wangu?* **2 *Samweli* 11:11**

Ulikuwa ni wakati wa vita. Wafalme walitarajiwa kuwa kwenye uwanja wa vita! Mfalme Daudi, hata hivyo, akaamua kupumzika na hilo likapelekea kilele cha anguko lake kimaadili. Watu wazembe huanguka dhambini. Kama Daudi angeenda vitani, asingemwona Bethsheba akioga na kuanguka kwenye dhambi ya zinaa naye. (Angalau angewaombea maaskari…., hata hivyo, ilikuwa jioni, wakati wake wa kuomba! **Zaburi 55:17**)

Shetani anaongea zaidi na watu wasiokuwa na shughuli yoyote. Ni bora kujishughulisha na mambo ya Mungu. Kujikwaa kwenye njia yenye mteremko mrefu hakuishii kwenye anguko moja. Tunaanguka na kuviringika! Hiki ndicho kilichomtokea Daudi. Ili kufunika dhambi yake moja, akatenda dhambi nyingi zaidi! Kiujanja akamwambia askari wake Uria, Mhiti, mumewe Bethsheba, kwenda nyumbani na kukaa na mke wake Kumbuka alikuwa mhiti, hakuwa Mwisraeli kamili.

Hata hivyo, akamwambia, *"Sanduku na Israel na Yuda, wanakaa vibandani; na Bwana wangu Yoabu, na watumishi wa Bwana wangu, wamepiga kambi waziwazi uwandani; nami niende nyumbani kwangu, kula na kunywa, na kulala na mke wangu? 2 samweli 11:11*

Tazama jinsi alivyokuwa mtiifu kwa kazi yake!
Hakufikiria chochote, ila vita! Raha zake mwenyewe hazikumgusa… Hapa, ni swali linalomkabili Daudi… Mfalme Daudi, uliwezaje kula, kunywa na kujifanyia anasa mbaya wakati watu wako wamepiga kambi uwandani kukukamatia mateka?

Ulidiriki hata kujipatia anasa kinyume na sheria, wakati Uria aliamua kukataa vitu vya kawaida kama chakula, vinywaji nyumbani kwake na hata kulala na mke wake….Tunaona jamii zinazopenda anasa zikituzunguka.

Na watu kama Daudi, watu wakuu wa Mungu, mtu "aliyependwa na Mungu" wanatafuta anasa zao! "kuna tatizo gani katika kuyafurahia maisha?" wanauliza. Jibu ni kwaba vita ya Bwana haijamalizika ….twawezaje?

**Maombi:** *Bwana, ninajua ya kuwa siwezi kuendekeza anasa za kidunia wakati vita vya Bwana havijamalizika. Nisaidie kushughulika na mambo ya Kimungu, AMINA.*

**Kwa usomaji zaidi: 2 Samweli 23 13-17, 1 Wakorintho 7. 29-31**

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Roho Yenye Kutakabali au Kiburi** - Njia ya anguko.

**Kifungu Cha Kusoma: Obadiah. 1- 21**

*"kiburi cha moyo wako kimekudanganya, wewe ukaaye katika pango za majabali, mwenye makao yako juu sana"* ***Obadia 1:3***

Titanic, meli kubwa na ya starehe zaidi iliyokuwa ikielea mara, ikazama mnamo tarehe 15 Aprili, 1912 wakati wa safari yake ya kwanza. Ilikuwa na kumbi mbili zilizogawanyika kwenye vyumba 16 visivyoweza kuingia maji.Ilidhaniwa haiwezi kuzama. Waundaji wa Titanic walidai, hakuna nguvu duniani inayoweza kuzamisha hiyo meli. Hawakujali hata kuchukua boti zaidi za kuokoa maisha kwa safari yake ya kwanza. Hata hivyo, mda mfupi kabla ya usiku wa manane wa april 14, ikagonga barafu, na meli ikazama. Zaidi ya watu 1,500 kati ya 2,200 wakapoteza maisha, kwenye bahari ya atlantiki.
Ni nini kilichosababisha Titanic izame? Barafu? Hapana! Ninaweza kusema, ni kiburi! " kiburi hutangulia uangamivu, na roho yenye kutakabali hutangulia maanguko" mithali 16:18

Edomu ulikuwa ni mji ulio kilimani, uliokaa kwenye ufa wa Mwamba uliokuwa kama ngome asilia.Hakuna adui ambaye angeweza kuushinda mji, kwa sababu ulikuwa juu ya milima yenye miamba. Zaidi ya hilo, ulikuwa na mashujaa. (**mst 7**). Kwa hiyo, Edomu alisema, " hakuna atakayeweza kunishusha"(**mst 3**)
Unafikiri unaishi juu ya "mlima mrefu," una nafasi nzuri ofisini kwako, kwenye taasisi, au kanisani? Unafikiri unaishi kwenye ufa wa mwamba, kama utajiri, afya, hekima? Labda una mashujaa… mvuto kwenye utawala, na wanasiasa…

Ingawa unaonyesha unyenyekevu kwa nje, labda una kiburi ndani ya moyo wako. Huwezi kumlaghai Mungu! Mungu anasema…"ijapokuwa kioto chako kimewekwa kati ya nyota, nitakushusha kutoka huko" (**mst 4**) "Kiburi cha moyo wako kimekudanganya", asema Bwana! Kiburi kinafanyika udanganyifu kwa sababu hakisikii maonyo! "Mashujaa" vile vile waliudanganya Edomu. Kuangamia kwake kulikuwa hakuepukiki! Tunapokuwa na kila kitu na kila mtu pamoja nasi, tunajiamini na kukataa maonyo! Lakini huo ni udanganyifu.Mtu mwenye roho ya kutakabari hawezi kumpendeza Mungu. "Naam ninyi nyote, jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana, kwa sababu, "Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema" Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake.(1 Petro 5:5-6)

**Maombi:** *Bwana, naomba nisidanganyike na mali, cheo au ushujaa. Naomba nijue kwamba mimi ni mavumbi na majivu, AMINA.*

**Kwa Usomaji zaidi: Matendo 12. 19- 23; Danieli 4. 1-36;**

Siku ya 27

# *MIGUUNI PA YESU*

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Roho ya Bwana iwe juu yako**.

**Kifungu Cha Kusoma: Hesabu 11:16-17; 24-30**

*"Ndipo Bwana akashuka ndani ya wingu, akanena nae, akatwaa sehemu ya roho iliyokuwa juu ya Musa, akaitia juu ya wale wazee sabini, ikawa, roho hiyo ilipowashukia, wakatabiri, lakini hawakufanya hivyo tena.* ***(Hesabu 11:25)***

Mtu wa leo hawezi kutulia na hata uwezo wa kuzingatia juu ya kitu chochote ni sifuri! Hawezi hata kutazama idhaa moja ya televisheni kwa zaidi ya saa moja. "Udadisi unampelekea asipumzike kubadilisha idhaa) na haturuhusu chochote" kitulie au kije juu" yetu.

Mungu alimwambia Musa, achague wazee 70 kutoka kwenye kusanyiko la wana Waisraeli, ili aweze kumimina roho yake juu yao. Alifanya hivyo na Roho ilipowashukia, wakatabiri! Roho inapaswa kutushukia. Hapo ndipo atafanya kazi kwetu. Kama mtawala wa jimbo lako akija nyumbani kwako kukusaidia… kutoa zawadi ya rehema, utafanya nini? Je hutamkaribisha? Umkarishe mahali pazuri, umpe kinywaji, na umpumzishe? Hapo tu ndipo, atafanya yaliyomleta.

Kadhalika Roho, vilevile, anatafuta kupumzika kwako.Neno "kupumzika" hapa linamaanisha "kutulia " katika mazingira ya asili. Pia lina maana ya 'kulala' au 'kusinzia'. Linatuambia nini basi? Lina maanisha Roho ajisikie kuwa na faraja ndani yako. Hapo ndipo anaweza "kutulia." Ni kama kumbeba mtu mabegani mwako na kuanza kutembea. Ukiendelea kutembea, mtu aliye begani kwako hawezi kupumzika.

Kwa nadra tunazingatia juu ya Mungu. Tunamwomba Roho aje juu yetu, ila mara chache tunaandaachumba kwa ajili yake. Hata tunapokaa katika uwepo wake Bwana miili yetu inatulia pale ila akili zetu zinazunguka zunguka sehemu zaidi ya mia moja. Je Roho awezaje kutulia juu yetu? Kumbuka, kila mara akili zetu zinapokweda kwenye vitu vya kidunia, ni kikwazo au kizuizi kwa Roho kutulia juu Yetu "kulala" Vilevile, kumbuka, Roho haji tu kusaidia na kuondoka. Anakuja kuishi pamoja na wewe, na kuwa msaada wa kudumu maishani mwako. Ni mwepesi sana kuhisi.ni lazima uwe mwepesi kumhisi Roho. Kama akisumbuliwa, anaweza akaondoka.

**Maombi:** Bwana*, nimeelewa Roho wako anatafuta kupumzika kwangu O Mungu! Na niwe mwepesi kumhisi Roho, Amina!*

**Kwa Usomaji Zaidi: Waefeso 4. 30-32; Mathayo. 12. 30-32**

**Anayeepukana na Uovu….**

**Kifungu Cha Kusoma: Ayubu 1:1-22**

*"Kwa kuwa hapana mmoja aliye kama yeye duniani, mtu mkamilifu na uelekevu, mwenye kumcha Mungu, na kuepukana na uovu"* ***Ayubu 1:8-9***

Mwandishi anamtambulisha Ayubu kama mkamilifu. **(mst 1)** Mungu analishuhudia hilo. **(mst 8)** Shetani analikubali hilo (hakuukataa huo ukweli, ila alijaribu kwa uongo kumshtaki Ayubu kwa uelekevu wake kwa sababu ya maalumu.**(Mst 9-11**) Vitu vinne Mungu anavisema kumhusu Ayubu: mkamilifu, uelekevu, anamcha Mungu na anaepukana na uovu. Ni nini cha ziada anachoweza mtu kuomba katika maisha haya ya duniani!

Sehemu ya kwanza inazungumzia ukamilifu katika kila sehemu, kama ilivyokuwa kwa wanyama wa sadaka (**Walawi 1:3**). Mungu anatarajia tuishi katika utakatifu uliokamilika katika maisha binafsi, ya kifamilia, kanisa, taaluma na jamii kiujumla! Zaidi ya hayo, ni shughuli ya masaa 24. Hata adui asipate fursa ya kukukashfu. (**1 Timotheo 5:14**)

Ayubu alikuwa ni mtu mkamilifu, mtu mnyoofu-tabia kama ya mtoto! Alikuwa muwazi na mtu wa kawaida, hakuwa na cha kuficha. Alimcha Mungu. Maana yake ni nini? Alijua kwamba Mungu alikuwa akitembea naye na kumtazama kwa kila alichokifanya. Kuishi katika uwepo wa Mungu kila wakati katika maisha yake kulimsaidia kuishi maisha matakatifu.

Mwisho, alikuwa ni mtu aliyeuepukana na uovu. Yamkini wewe ni mkamilifu na unamcha Mungu, unaishi maisha makamilifu, bado unatakiwa kukaa mbali na hali zote za dhambi. Wapo watu waishio maisha matakatifu, lakini hakuna awezaye kukwepa majaribu!

Kuepukana na uovu ni tendo la makusudi. Ni kuazimia kwamba hautajinajisi. Ayubu anasema "nilifanya agano na macho yangu, basi nawezaje kumwangalia msichana?" **Ayubu 31:1** Nadhiri ya Ayubu haikuwa kutokuzini tu, lakini kwamba angejiepusha kutoka kwenye maeneo au mazingara yote ya tamaaambayo yangepelekea anguko lake. Sio agano na macho yetu. Msimamo ni kufanya agano na viungo vyote vya mwili wako, na vitivo vyote vinavyomwaga fikra ndani ya akili zako, na vimeng'enya vyote vinavyochochea hisia moyoni mwako!

**Maombi:** *Bwana, nisaidie kuishi maisha makamilifu, ya uelekevu na ya kumcha Mungu. Nisaidie nikupendeze wewe, AMINA*

**Kwa usomaji Zaidi: Danieli 1. 3-20 1 Thesalonike. 5 21-22**

Siku ya 29

# MIGUUNI PA YESU

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Ushuhudiaji: Msukumo wa Ndani**

**Kifungu cha kusoma: Yohana 1: 35-51**

*Huyo akamwona kwanza Simoni, ndugu yake mwenyewe, akamwambia, tumemwona Masihi (Maana yake, Kristo). Akampeleka kwa Yesu."* ***Yohana 1:41-42***

Yohana Mbatizaji alimtambulisha Yesu kama mwana kondoo wa Mungu anayezichukua dhambi za ulimwengu! Kwa kusikia ushuhuda huu, wanafunzi wawlili wa Yohana, wakamwendea Yesu na hata kukaa naye kwa siku ile. Wakashawishika kwamba Yesu alikuwa Masihi. Walipokuwa wanarudi, Andrea, mmoja wa wanafuzi, akampata kaka yake Simoni. (Andrea alikuwa, kwa hakika, akimtafuta Simoni).

Biblia ya NIV inalisema hili kwa usahihi….kitu cha kwanza alichokifanya Andrea ni kutafuta. Andrea alisisimka. Hakuweza kutuliza furaha yake ya kuitafuta hazina yaani Yesu Masihi! (Mathayo 13:44) Akaanza "uinjilisti" akashuhudia, na hata akamleta ndugu yake kwa Yesu na hilo likapelekea wokovu wa Simoni! Andrea hakungojea shahada ya theolojia ili aanze ushuhudiaji. Hakungojea "mkutano mkubwa wa injili" kwenye jukwaa au hata karama za kiroho ili ushuhudiaji wake uwe na matokeo mazuri. Aliumwaga moyo wake kwa ndugu yake!

Kushuhudia ni kuwaambia wengine ulichokipata….kwa Yesu. Unapofanya hivyo kutoka moyoni, ndivyo ilivyokuwa! Wote waliompata Yesu na kukaa pamoja naye angalau kwa siku moja hawawezi kuacha kushuhudia.

Andrea akaanza kushuhudia asubuhi iliyofuata baada ya kumpokea Yesu. Hakusubiria "fursa kubwa." Akaanza na ndugu yake mwenyewe. Anza na kidogo. Kuwa mwaminifu katika madogo ni kitu kikubwa. Kwake yeye, ndugu yake alikuwa wa muhimu.

Ukweli nilioupata, ndugu yangu ni lazima aupate vilevile…hiyo ndiyo ilikuwa akilini mwake. Ushuhudiaji lazima uwe msukumo wa ndani. Labda Andrea hakuwa mhubiri mkubwa. (Kuhubiri, wakati fulani, ni shughuli ya akili ambapo maneno ni muhimu. Ushuhudiaji, kwa upande mwingine, ni shughuli ya moyoni na maneno sio muhimu kiasi hicho.) Lakini ni Andrea ndiye aliyemleta kijana mdogo aliyekuwa na mikate mitano na samaki wawili kwa Yesu. (Yohana 6: 8-9).

Vivyo hivyo, mwongofu wa kwanza wa Andera –Simoni Petro, ndugu yake- alikuwa mhubiri mkubwa na alileta roho 3,000 kwenye mafundisho yake ya kwanza. Nina uhakika Andrea atapokea sehemu ya thawabu ya watu wale waliookoka siku ya Pentekoste!

**Maombi:** *Bwana, nisaidie nikushuhudie, kila mahali, kila wakati. AMINA!*

**Kwa usomaji zaidi:** Warumi 1. 16-20; Yohana 4: 28-42.

Siku ya 30

# *MIGUUNI PA YESU*

*Kuwepo mbele za Bwana kila siku*

**Umetengwa ….kwa ajili ya Mungu Mwenyewe.**

**Kifungu cha kusoma: Zaburi. 4: 1- 8**

*"Bali jueni ya kuwa Bwana amejiteulia mtauwa"* ***Zaburi 4:3***

Tunaelewa kuwa sisi ni watu tuliotengwa, tulioitwa kutoka gizani… Tunasema, tulikuwa kwenye shimo refu, kwenye udongo wenye matope, bila tumaini….Tunaongelea tu sehemu tulizokuwa, kwenye hatua ya anguko; na vilio tulivyolia… Tulitaka tu kuwa huru kutoka kwenye kifungo kwenda sehemu nyingine yoyote… na Yesu akatukomboa.

Hata hivyo, Je huo ndio mwisho wa habari? Hapa, mwandishi wa zaburi anasema, Bwana hajatukomboa tu, bali pia ametutenga kwa ajili yake. Anaanza na kauli ya, "bali jueni… ", kwa sababu; tunasahau ukweli huu mara nyingi!

Mungu hakuokoi na kukuacha peke yako, mahali Fulani uliokookolewa kutoka kwenye shimo. Anakufanya kuwa Wake! Kwa nini Mungu anatutenga kwa ajili yake! Kwa sababu tulianguka kutoka kwake, Tulianguka kutoka kwake (tulimwacha) kwenda dhambini, gizani, kusiko na tumaini na mautini! Mbali na Yeye tunakuwa wahanga kwa shetani. Kutengana na upendo Wake tuliingia kwenye ulimwengu wenye ghadhabu ya Mungu kwa hiyo, hata kwa habari ya wokovu wetu, tunahitaji kurudi kwake. Kama tukishindwa kutengwa kwa ajili ya Mungu, wokovu wetu haujakamilika!

Tulikuwa watu Wake, tukapotea. Sasa tumerudishwa… sasa mimi sio yatima. Nimerudi nyumbani kwa Baba yangu! Na sasa, ninahitaji kuishi na Baba yangu. Ninaelewa kuwa, mbali na wewe, mimi ni yatima. Siko salama….Kwa hiyo, ninachokifanya ni kuishi karibu naye ili chochote kisinitenge na upendo Wake wa milele!

Mungu alipotaka kuwateua au kuwachagua watu wachache kumsaidia Musa katika kazi za utawala, alimwambia Musa "nikusanyie watu sabini, miongoni mwa wazee wa Israel" (**Hesabu 11:16**). Hata Yesu alipowachagua kumi na wawili, ilikuwa wawe pamoja nae, na waagizwe kwenda kuhubiri (**Marko 3:14)**

"Kondoo zangu, kondoo za malisho yangu, ni wanadamu na mimi ni Mungu wenu, asema Bwana Mungu" (**Ezekiel 34:31**). Ndiyo, mlikuwa mnapotea kama kondoo, lakini sasa mmemrudia mchungaji na mwangalizi wa roho zenu" (**1Petro 2:25**). Na tukumbuke, kila wakati katika maisha yetu, sisi ni Wake.

**Maombi:** *Ee BWANA, utugeuze kwako, nasi tutageuka! (Maombolezo 5:21)*

**Kwa usomaji zaidi:** Zaburi 23; Yohana 13:22-25